



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**TAARIFA KWA UMMA  
KUHUSU PATO LA TAIFA  
KWA ROBO YA PILI YA MWAKA  
(APRILI – JUNI), 2014**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha  
Oktoba, 2014**

## 1.0 Utangulizi


Taarifa za takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka zinatumiwa katika kutathmini mabadiliko ya ukuaji wa uchumi katika vipindi vifupi vya robo mwaka. Taarifa hii ni kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2014.

Taarifa zilizotumiwa katika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa zimetokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma Nchini katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014. Aidha, ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa umezingatia matakwa ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa (UN System of National Accounts).

### 1.1 Ukuaji wa Pato la Taifa

Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei ya soko uliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2013, **(Kielelezo Namba 1.)** Jumla ya thamani ya Pato la Taifa katika kipindi husika ilikuwa Shilingi 5,402,531 milioni mwaka 2014 ikilinganishwa na Shilingi 5,055,349 milioni mwaka 2013.

**Kielelezo Namba 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo ya Pili ya Mwaka, (Aprili – June) 2004 – 2014**



## **2.0 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi**

Mchanganuo wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwenye Pato la Taifa kwa robo ya pili ya mwaka 2014 ni kama ifuatavyo:

### **2.1 Kilimo na Uvuvi**

Shughuli za kiuchumi za kilimo zilikua kwa kasi ya asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Katika kipindi hicho, Shughuli za Kilimo cha Mazao zilikua kwa asilimia 6.5 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2013; Shughuli za Mifugo zilikua kwa asilimia 0.9 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 3.8 na Shughuli za Misitu na Uwindaji zilikua kwa asilimia 0.8 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2013. Aidha, katika kipindi hicho kulikuwa na mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha mazao kwa wingi, pia upatikanaji wa ruzuku ya pemebejeo na maelekezo ya ma-ofisa Ugani kwa wakulima.

Shughuli za uvuvi zilikua kwa kasi ya asilimia 2.1 katika robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 2.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kasi ya ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa uvunaji wa samaki ili kukidhi mahitaji ya samaki katika soko la ndani na soko la kimataifa.

### **2.2 Viwanda na Ujenzi**

Shughuli za uchimbaji madini, mawe na kokoto ziliongezeka na kufikia kasi ya asilimia 3.0 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia hasi 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kuongezeka kwa kasi hii ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya almasi na Tanzanite katika robo ya pili ya mwaka 2014. Aidha, uzalishaji wa dhahabu ulipungua katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014.

Shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa kasi ya asilimia 7.0 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.6 mwaka 2013. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji na uhifadhi wa bidhaa za nyama, samaki, matunda, mboga za majani na mafuta. Shughuli nyingine zilizochangia katika ukuaji ni pamoja na uzalishaji wa bidhaa nyinginezo za vyakula, nguo na simenti.

Shughuli za uzalishaji nishati ya umeme na usambazaji maji zilikua kwa kasi ya asilimia 7.7 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kuongezeka kwa ukuaji wa nishati ya umeme na maji kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa nishati ya umeme unaotokana na mafuta na gesi.

### **2.3 Shughuli za Uchumi za Utoaji Huduma**

Shughuli za biashara ya jumla na reja reja, ukarabati wa magari na pikipiki na vifaa vingine vya nyumbani zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 7.1 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.6 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2013. Shughuli za upangishaji nyumba, na shughuli zingine za biashara zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 6.5 ukilinganisha na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Shughuli za uchukuzi na mawasiliano zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 16.8 katika kipindi husika. Shughuli nyingine ni huduma za Hoteli na migahawa zilizofikia kasi ya ukuaji wa asilimia 4.0; Shughuli za uendeshaji Serikali zilifikia kasi ya asilimia 4.8, Elimu asilimia 6.3 na huduma za Afya na shughuli nyinginezo zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi hicho.

### **3.0 Hitimisho**

Pato la Taifa limetayarishwa kutokana na taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli za kiuchumi katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2014, na limekua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 7.6 katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2013.

Kwa mujibu wa shajala ya machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu za Pato la taifa kwa robo ya tatu ya mwaka 2014 itasambazwa tarehe 31, Desemba 2014.